

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA AFYA TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UGONJWA WA MPOX

Tarehe 19 Agosti, 2024.

Ndugu wananchi, mnamo tarehe 17 Agosti, 2024, Wizara ya Afya ilitoa taarifa kwa Umma kuhusu Ugonjwa wa Mpx kufuatia kuongezeka kwa visa duniani ikiwemo baadhi ya nchi za Afrika Mashariki na kuujulisha umma uchukue tahadhari ili kuhakikisha ugonjwa huu hatingii nchini.

Ndugu wananchi, kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Afya Duniani (WHO), ugonjwa wa Mpx umeendelea kuenea katika nchi mbalimbali duniani. Kwa takwimu za kipindi cha tarehe **1 Januari 2022** hadi **30 Juni 2024**, jumla ya wagonjwa **99,176** wamethibitika kuwa na Mpx katika nchi **116** duniani ambapo watu **208 sawa na asilimia 0.2 walipoteza maisha kwa sababu ya ugonjwa huu**. Kati, ya visa vyote duniani, **bara la Afrika limethibitisha visa 4,232 sawa na asilimia 4.3 ya wagonjwa wote duniani**. Mabara yanayoongoza kuwa na visa vingi ni **Amerika ya Kaskazini na Kusini** yakiwa na visa **62,904 sawa na asilimia 63.4** yakifuatiwa na **Bara la Ulaya** lenye visa **27,529, sawa na asilimia 27.8** ya visa vyote duniani.

Ndugu Wananchi, napenda kuwajulisha kuwa, **mpaka sasa hakuna mgonjwa ye yote aliyethibitika kuwa na maambukizi ya Mpx nchini**. Wizara ya Afya inaendelea kuchukua hatua zifuatazo kuzuia ugonjwa wa Mpx kuingia nchini:

- i. Kuimarisha uchunguzi kwa wasafiri kuitia huduma za Afya Mipakani ikiwemo bandari, nchi kavu na viwanja vya ndege, ili kubaini wasafiri wenye viashiria na dalili za ugonjwa huu na kuchukua hatua stahiki.
- ii. Kufuatilia katika jamii mtu ye yote mwenye viashiria au dalili za ugonjwa huu ili kumhudumia kwa haraka na kupunguza kusambaa kwa maambukizi endapo ugonjwa utaingia nchini.
- iii. Kwa kushirikiana na Timu za Afya za Mikoa, Halmashauri, watoa huduma ngazi ya jamii na katika vituo vya kutolea huduma za afya, tumeimarisha utayari katika vituo

vya kutolea huduma za afya, maabara za uchunguzi, upatikanaji wa dawa, vifaa kinga na tiba ili kutoa huduma stahiki endapo ugonjwa utaingia nchini.

- iv. Kutoa elimu kwa njia mbalimbali ikiwemo Televisheni, Radio na Vipeperushi katika mitandao ya kijamii na kuujulisha umma juu ya mwenendo wa ugonjwa huu ili kuchukua hatua stahiki.

Ndugu Wananchi, ni wajibu wa kila mmoja kuchukua hatua za tahadhari **ili nchi iendelee kuwa salama.** Hivyo, naomba kila mmoja aendelee kuzingatia yafuatayo:

- i. **Kuwahi katika vituo vya kutolea huduma za afya** unapoona dalili za ugonjwa wa Mpox. Mfano, homa inayoambatana na vipele kwenye sehemu za mwili, kuchoka na kuvimba mtoki.
- ii. **Kutoa taarifa za watu wenyewe viashiria au dalili za ugonjwa wa Mpox** kwa kupiga bure namba 199 kwa ajili ya kupata huduma.
- iii. **Kuepuka kugusana** kwa njia ya kusalimiana kwa kupeana mikono, kukumbatiana, kujamiiiana na mtu mwenye dalili za Mpox au kugusa majimaji ya mgonjwa wa Mpox.
- iv. **Kunawa mikono** kila mara kwa maji tiririka na sabuni au kutumia vitakasa mikono. Katika hili nitoe wito kwa maeneo ya umma, kaya na taasisi mbalimbali ikiwemo shule, vyuo na vituo vya kutolea huduma za afya kuhakikisha kunakuwa na vifaa vya kunawia mikono vyenye maji tiririka na sabuni ili kurahisisha unawaji wa mikono.
- v. **Kusafisha na kutakasa vyombo vilivyotumika** na mtu mwenye dalili za Mpox pamoja na maeneo yote yanayoguswa mara kwa mara kwa kutumia sabuni au Klorini (mfano Jik).
- vi. Epuka kula au kugusa mizoga au wanyama ambao wanaweza kuwa na maambukizi.
- vii. Vilevile, vaa barakoa kwa tahadhari iwapo itabidi kukaa na kuongea kwa karibu na mtu mwenye dalili za Mpox.

Ndugu wananchi, napenda kuwatoa hofu kuwa bado nchi iko salama. Hivyo, natoa wito kwa wataalam wa afya nchini na jamii kwa ujumla kushirikiana kuhakikisha nchi yetu inabaki kuwa salama.

Asante kwa kunisikiliza.

Imetolewa na: Jenista Mhagama (Mb)
WAZIRI WA AFYA
19 Agosti, 2024